# Tanzania yaonesha njia Mission 300

mjasiriamali @mjasiriamali @mjasiriamali

MJASIRIAMALI

KAMATA FURSA

Tovuti www.mjasriamari.co.tz/ ISSN 3456-1679. Na. 14, Ijumaa Januari 31, 2025 Bei Tsh. 1,000/= Ksh 100


HUU NI ZAIDI YA UWEKEZAJI...

# Sh. Trilioni 33 za Dk Samia

- WAJASIRIAMLI WADOGO WASEMA UTAKUWA NI UKOMBOZI MKUBWA KWAO
- WAKIRI CHANGAMOTO NISHATI YA UMEME NI KIKWAZO KIKUBWA
- WACHUMI WAKIRI KUPANGA NI KUCHAGUA, AMECHEZA KARATA YAKE VYEMA



## Zanzibar mguu sawa Uwekezaji



## Njiwa si uchawi, fuga utoboe!

# Uthubutu wa Dk Samia wapagawisha

NA MWANDISHI WETU

**HUU utakuwa zaidi ya uwekezaji, kwani wananchi mbalimbali bado wameendelea kuguswa na kitendo cha Dk. Samia Suluhu Hassan, kuwekeza kwenye nishati ya umeme kwa kutumia kiasi cha Sh trilioni 33.**

Fedha hizo zitawanufaisha Watanzania wote kwani zinaenda kutibu tatizo la umeme nchini, ambapo kaya zaidi ya milioni 8.3 zitakuwa na uhakika wa kupata umeme na kuondokana na giza.

Wananchi kadhaa waliozungumza na gazeti hili walisema, uhakika wa umeme ni ukombozi kwa kila Mtanzania, kwani kwa dunia ya sasa ya sayani na teknolojia, nishati ya umeme ni kitu cha lazima.

"Hiki kinachokwenda kufanyika ni zaidi ya uwekezaji, wengine wanaweza wasielewe, mfano mimi natoka Mbinga na katika kitongoji chetu hakuna umeme, najua tabu wanazopata wakazi wa pale.

"Nina utaalamu wa mambo ya saluni, lakini nashindwa kufungua chochote kule zaidi ya kukimbia na kuja mjini kuhangaika, huyu Mama (Dkt. Samia), Mungu tu amzidishie," alisema Eva Kapinga mkazi wa Buza, Dar es Salaam.

Katika mahojiano yetu na watu wa kada ya chini na kati, haswa wajasiriamali, walikiri tabu wanayoipata katika umeme wengi hawaijui na wanaweza kusoma katika vitabu au makaratasi na kutoelewa vile wanavyopata shida kwa suala hilo.

"Nipo hapa Masumbwe huku Geita, nimelazimika kuishi katika mji huu maana natoka mbugani (shambani) huko hakuna umeme na tunapata shida, inakuwa tabu kurudi hata nyumbani kuanzisha chochote kile.

"Nilimsikia Mama alichosema, nilijiuliza hii ni ndoto au itakuja kuwa kweli? Yaani anakwenda kutupa raha, anatupa raha ambayo hatunayo kwa sasa,' alisema Maganga Fikiri.

Baadhi ya wachambuzi wa uchumi wameshatamka wazi na kukaririwa wakisifu mpango huo na kusema, uwekezaji unaokwenda kufanyika ni tiba tosha kwa nchi hii.

"Usione vyaelea vimeundwa… hii ndio maana yake, tunataka biashara ya umeme, lazima tuwekeze, nina hakika rais amepata ushauri mzuri ndio maana ameingia kuwekeza, wote walioendelea kwenye biashara hii waliwekeza na rais anawekeza sasa, kupanga ni kuchagua, kama fursa imeonekana kwenye nishati hakuna budi kuitumia.

"Ili uendelee unahitaji kuwa na nishati ya uhakika, nchi zote zenye maendeleo zina nishati ya uhakika na waliwekeza kwenye hilo, uchumi utakua na unajua diplomasia ya uchumi ina nafasi kubwa sana katika kuunganisha mataifa hata Umoja wa Ulaya mambo ya uchumi ndiyo yaliunganisha," alikaririwa mchambuzi wa masuala ya uchumi Walter Nguma.

Tanzania inatarajiwa kufanya makubwa kwenye sekta ya ajira na uwekezaji kutokana na Azimio la Dar es Salaam katika mkutano wa nishati wa Misheni 300 uliomalizika Dar es Salaam Januari 28.

Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alisema Azimio la Dar es Salaam litakuwa chachu ya ukombozi wa kiuchumi Afrika.

Mchumi mwingine alisema; "Tuna zaidi ya megawati 3000 lakini kwa matumizi ya Tanzania ni takribani megawati 1,800 hivi kwa hiyo tuna umeme wa ziada kuuza nje, hii itatusaidia kupata nafuu ya umeme kwani tukiuza vizuri itatuletea mapato," alisema Nguma.

Imeelezwa mkutano wa Misheni 300 una faida kubwa kwani umeme ni kiungo muhimu kwenye matumizi ya kila siku na hata katika sekta ya elimu.

"Pia, itavutia vijana kufanya kazi mahali popote iwe vijijini au mijini sababu ya nishati ya umeme, pia watu wanaweza kujiajiri, pia kuvutia wawekezaji lazima watahitaji nishati kwenye mambo ya kilimo cha umwagiliaji."

# Zanzibar mguu sawa uwekezaji

NA MWANDISHI WETU, Z'bar

**KATIKA kile kile kinachoonekana kujiimrisha zaidi katika uwekezaji Serikali ya Zanzibar, imejipanga kuweka mazingira mauri zaidi katika uwekezaji viiwani humo.**



Hii yote ni kuhakikisha wakazi wa Zanzibar na Watanzania kwa ujumla wanafaidika na matunda ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ambayo yalikuwa na lengo la kumtoa mwananchji wa kawaida katika ukandamizaji na unyonyaji.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la seMapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amethibitisha hilo na kusema Zanzibar itaendelea kuweka mazingira mazuri zaidi ya kuwavutia wawekezaji zaidi ya uwekezaji hapa nchini.

Rais Dkt. Mwinyi alitoa hakikisho hilo hivi karibuni, wakati alipozungumza na Balozi wa Tanzania nchini, Celestine Kakele aliyefika Ikulu kujitambulisha.

Kutoa hakikisho hilo, Rais Dkt. Mwinyi ameeleza kuwa kuna fursa kubwa ya nchi hizo mbili kushirikiana hasa katika Sekta ya Utalii na Uwekezaji ambazo zikifanyika vyema nchi hizo zinaweza kunufaika kwa kiasi kikubwa.

Dk. Mwinyi amemsisitiza Balozi Kakele kufanya juhudi maalum za kuwavutia wawekezaji kutoka Nigeria kuja kuangalia fursa za Uwekezaji na Serikali inaandaa Mazingira mazuri ya kuwa na Uwekezaji wenye tija na Endelevu.

Amemuhakikishia Balozi huyo kuwa Serikali inaimarisha Uwekezaji kwa kuondoa vikwazo vinavyozorotesha ushirikiano kwa lengo la kuwavutia wawekezaji.

Amefahamisha kuwa utalii na uwekezaji ni vichocheo muhimu vya uchumi wa Zanzibar hivyo ni vema akaweka mkazo katika kuwavutia wawekezaji katika maeneo hayo.

Rais Dkt. Mwinyi ameilezea Sekta ya Biashara kuwa ni eneo jengine ambalo nchi hizo mbili zinaweza zikashirikiana katika kuuziana bidhaa za ndani, huku akisema bidhaa nyingi toka Afrika Magharibi zinauzwa nje ya Afrika kuliko zile zinazouzwa katika Ukanda wa Afrika.

Naye Balozi Kakele amesema Nigeria ina fursa nyingi ambazo Tanzania ikiwemo Zanzibar zinaweza kushirikiana hususani uwekezaji katika biashara na huduma za kibenki na kushauri kuandaliwa mazingira wezeshi ya upatikanaji viza baina ya nchi hizo.

# Watakiwa kutumia Nishati mbadala

NA MWANDISHI WETU

**MKUU wa Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma Mheshimiwa Kapenjama Ndile amewataka wananchi kuachana na matumizi ya kuni na badala yake kutumia nishati mbadala kwa ajili ya kupikia ili kudhibiti uharibifu wa mazingira, kupunguza hatari ya jangwa, na kuhifadhi uoto wa asili.**

Kapenjama amesema haiyo katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya ya Songea (DCC) kilichofanyika katika ukumbi wa HOMSO Songea.

Wadau mbalimbali walihudhuria kikao hicho kwa lengo la kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa kazi kupitia halmashauri za Madaba, Songea, na Manispaa ya Songea.

Miongoni mwa sekta zilizojadiliwa ni pamoja na utoaji wa elimu kwa jamii kuhusu matumizi sahihi ya nishati mbadala kama makaa ya mawe, mikakati ya kudhibiti utoro wa wanafunzi katika shule za msingi na sekondari, na udhibiti wa ufugaji holela wa ng'ombe.

Afisa Misitu wa Manispaa ya Songea, Betram Njelekera, amesema kuwa kwa kuunga mkono jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita, Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini amewezesha vikundi 12 kwa kuwagawia mama lishe mitungi 84 ya gesi ili kusaidia kupunguza uharibifu wa mazingira.



# Biteko anena mitaala ya Teknolojia

NA MWANDISHI WETU

**VYUO na taasisi zinazotoa elimu ngazi ya Kati ikiwemo Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), zimetakiwa kuboresha mitaala yake ya masomo ili iendane na mahitaji ya sasa ya soko la ajira kimataifa sambamba na mahitaji ya kijamii na kiuchumi.**

Hayo yamebainishwa jana na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko katika Maadhimisho ya miaka 60 ya chuo hicho kilichoanzishwa Januari 21, 1965.

"Serikali inasisitiza matumizi ya teknolojia za kisasa na mbinu za kujifunza zinazojibu changamoto za kimataifa, " Amesema Dkt. Biteko.

Amesema kuwa Serikali inazitaka taasisi za elimu ya kati kikiwemo Chuo cha CBE kuweka mkazo kwenye mafunzo ya ujasiriamali, ili wahitimu wake waweze kuchangia kikamilifu katika uchumi wa taifa kupitia biashara bunifu na ajira binafsi.

Aidha, taasisi za elimu, zikiwemo vyuo kama CBE, amezitaka kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi ili kuhakikisha mafunzo yanayotolewa yanakidhi mahitaji ya soko la ajira na pia kusaidia kukuza sekta hiyo kwa utafiti na mafunzo.

Ameongeza kuwa, Serikali inahimiza vyuo vya elimu ya biashara kufanya tafiti za kina zinazosaidia kutatua changamoto za kiuchumi, kuimarisha sera za biashara, na kubuni suluhisho endelevu.

"Serikali imeelekeza taasisi kama CBE zihakikishe kwamba fursa za elimu zinafikia makundi yote ya jamii, wakiwemo wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu, ili kuongeza ushiriki wa makundi yote katika uchumi wa taifa, " ameongeza Dkt. Biteko.

Naye, Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Selemani Jafo amesema CBE ni kitovu cha biashara nchini na kimeweza kujenga mahusiano na nchi mbalimbali kimataifa ikiwemo nchi ya China na Ujerumani na ni ufunguo wa ufanyaji wa biashara katika kampasi zote nchini.

Kwa upande wake, Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba amesema CBE imekuwa ikifanya kazi nzuri na kina mchango mkubwa katika ukuaji wa sekta ya fedha hapa nchini.

"Fedha na Biashara na Uwekezaji havitengamani lakini mafanikio yote yaliyofikiwa lazima tumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono na uongozi wake uliotuheshimisha, " Amesema Mhe. Nchemba.

Vilevile, Mkuu wa Chuo cha CBE, Prof. Edda Lwoga amesema kuwa katika maadhimisho ya miaka 60 ya CBE wemekuwa wakitoa elimu ya biashara kwa makundi mbalimbali ya kijamii na pia wametoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau mbalimbali wa biashara.

# Mradi wa maji wapigwa tafu

NA ALBANO MIDELO, Songea

**KATIKA juhudi za kuboresha huduma za maji safi na usafi wa mazingira, serikali ya Tanzania imeanzisha Mradi wa Maji wa Miji 28, ambao unatekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini.**

Mji wa Songea mkoani Ruvuma ni miongoni mwa miji inayonufaika na mradi huu, kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa wakazi wake.

Mkurungezi wa Mamlaka ya Maji safi Songea (SOUWASA) Mhandisi Patrick Kibasa anasema Mkataba wa mradi huu ulisainiwa tarehe 10 Machi 2023 kati ya Wizara ya Maji na China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC) kwa gharama ya TZS Bilioni 145.77.

Anasema Utekelezaji wa ujenzi ulianza rasmi Januari 2, 2024, na hadi sasa maendeleo yamefikia asilimia tano

Kulingana na Kibasa Mradi huu umebuniwa ili kuongeza upatikanaji wa maji na kuboresha miundombinu ya maji safi kwa wakazi wa Songea ikiwemo Ujenzi wa miundombinu ya kudaka maji kutoka Mto Njuga katika kijiji cha Kikunja, Halmashauri ya Wilaya ya Songea.

Anasema mradi huo utaongeza uzalishaji wa maji hadi lita milioni 17 kwa siku.

# Wapambanaji kushikwa mkono

NA MWANDISHI WETU

**SERIKALI imekiri bado inaendelea na mpango wa kuwasaidia wajasiriamali kuzalisha bidhaa bora ili kupata masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi.**

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe amebainisha mpango wa Serikali katika kuwasaidia wajasiriamali kuzalisha bidhaa bora ili kupata masoko ya uhakika.

Kigahe alisema Serikali imeweka mipango kadhaa ya kuwasaidia wajasiriamali kuzalisha bidhaa bora ili kupata masoko ya uhakika ikiwa ni pamoja na kupitia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Hii ikiwa ni kuwasaidia wajasiriamali wadogo kupata maeneo pamoja na majengo ya kuzalishia bidhaa zao, kuwapatia mitaji kupita Mfuko wa NEDF na nembo ya ubora wa bidhaa zao kwa miaka mitatu bila gharama.

Amesema pia kupitia SIDO, TBS na Wakala wa Vipimo (WMA) wataendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali kuhusu kanuni za uzalishaji wenye tija, elimu ya utambuzi wa vifungashio na ufungashaji bora

Pia amesema SIDO kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) itaendelea kuandaa na kuratibu maonesho mbalimbali ndani na nje ya nchi ikiwa ni sehemu ya kuchagiza ukuaji wa soko la bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali.

Kigahe alisema, kwa sasa SIDO imekuwa na uwezo mdogo wa kuwezesha mitaji kwa wajasiriamali ambao wamekuwa wakiongezeka kila wakati.

# LINDA AFYA YAKO

## Umuhimu wa 'kubwia' Kabichi



**KABICHI ina lishe bora na yenye vitamini C, nyuzinyuzi, na vitamini K. Watafiti wanapendekeza kwamba inaweza kuwa na manufaa ya kiafya ambayo ni pamoja na kusaidia usagaji chakula na afya ya moyo, miongoni mwa mengine.**

Licha ya kuwa na virutubisho vyenye lishe ya kuvutia, kabichi mara nyingi hupuuzwa.

Ingawa inaweza kuonekana kama mboga za lettusi, kwa hakika ni aina ya mboga za Brassica, ambayo ni pamoja na broccoli na figili.

Huwa katika maumbo na rangi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na nyekundu, zambarau, nyeupe, na kijani, na majani yake yanaweza kujikunja au kuwa laini.

Mboga hii hulimwa duniani kote kwa maelfu ya miaka na inaweza kupatikana katika mapishi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na sauerkraut, kimchi na coleslaw. Zaidi ya hayo, kabichi imejaa vitamini na madini.

1. Kabichi imejaa virutubisho

Ingawa kabichi ina kalori chache sana, ina virutubishi vinavyovutia.

Kwa kweli, kikombe 1 tu, au gramu 89 (g), ya kabichi mbichi ya kijani ina lishe zifuatazo; Kalori, Protini, Nyuzinyuzi, Vitamini K, Vitamini C, Folate, Manganese, Vitamini B, Kalsiamu, Potasiamu na Magnesiamu. Kabichi pia ina kiasi kidogo cha virutubisho vingine, ikiwa ni pamoja na vitamini A, chuma, na riboflauini.

Kama unavyoona katika orodha iliyo hapo juu, ina vitamini B6 na asidi nyingi, zote mbili ni muhimu kwa michakato mingi muhimu mwilini, ikijumuisha Mabadiliko ya kemikali yanayotokea katika seli na utendakazi wa kawaida wa mfumo wa neva kwa mujibu wa wataalamu.

Kwa kuongezea, kabichi ina nyuzinyuzi nyingi na ina vioksidishaji vikali, ikijumuisha polyphenols na madini ya salfa.

Kabichi ina vitamini C nyingi,yenye nguvu inayosaidia kulinda mwili dhidi ya magonjwa ya moyo, aina kadhaa za saratani, na kupoteza uwezo wa kuona.

2. Inaweza kusaidia kudhibiti kuvimba

Kuvimba sio jambo baya kila wakati. Kwa kweli, mwili wako hutegemea vichocheo ili kujilinda dhidi ya maambukizi au kuharakisha uponyaji.

Aina hii ya kuvimba kwa papo hapo ni hali ya kawaida panapotokea jeraha au maambukizi.

Kwa upande mwingine, uvimbe unaotokea kwa muda mrefu unahusishwa na magonjwa mengi, ikiwa ni pamoja na ugonjwa wa moyo, ugonjwa wa kukakamaa viungo na ugonjwa wa maambukizi katika utumbo.

Mboga kama kabichi zina madini ambayo husaidia kupunguza kuvimba kwa muda mrefu.

Kwa kweli, utafiti mmoja wa 2014 uliojumuisha vijana walio na umri wa miaka 20-40 ulionyesha kuwa kula mboga za aina ya kabichi kunaweza kupunguza alama fulani za damu kuvimba.

Utafiti mwingine wa zamani kwa zaidi ya wanawake 1,000 ulionyesha kuwa wale waliokula kiasi kikubwa cha mboga za jamii ya kabichi walikuwa na viwango vidogo vya kuvimba, ikilinganishwa na wale waliokula kabichi kwa kiasi cha chini zaidi.

Sulforaphane, kaempferol, na vioksidishaji vingine vinavyopatikana katika kundi hili la mimea husaidia kuzuia makali ya kuvimba inapotokea jeraha au maambukizi.

Vitamini C, pia inajulikana kama asidi ascorbic, ni vitamini iliyokatika hali ya majimaji ambayo hufanya kazi nyingi muhimu katika mwili.

Kwa mfano, inahitajika kutengeneza collagen, protini nyingi zaidi mwilini. Collagen hutoa muundo na unyumbulifu kwa ngozi na ni muhimu kwa utendakazi mzuri wa mifupa, misuli na mishipa ya damu.

Zaidi ya hayo, vitamini C husaidia mwili kunyonya madini chuma, inayopatikana katika vyakula vya mimea.



## MAONI

### Wajasiriamali huu ni muda wa kupambana

**KUSEMA kweli kunaK fikra potofu zimejengeka miongoni mwa watu wakidhani kuwa kufanya kazi kwa bidii ni utumwa. Hii ni kutokana na dunia ya sasa kujaa watu wasiopenda kazi na wavivu.**

Huwezi kutumia muda vyema kama hutofanya kazi kwa bidii. Ukiwa na bidii katika kufanya kazi, unaweza kufanya kazi za siku nzima ndani ya saa moja au kazi za siku mbili ndani ya siku moja.

Hakuna mtu yeyote aliyefanikiwa bila kutumia muda vyema; muda ni mali, hivyo yakupasa uutumie vyema kwa kufanya kazi kwa bidii.

Kanuni moja wapo ya kufikia malengo ni kufanya kazi kwa bidii. Safari ya mafanikio siyo ya mteremko, inahitaji juhudi nyingi ili tuweze kuona matokeo.

Hakuna mtu aliyewahi kufanikiwa kwa kufanya kazi kivivu; fuatilia watu waliofanikiwa watakueleza jinsi wanavyofanya kazi usiku na mchana ili kukamilisha ndoto zao.


Nani atamheshimu mvivu? Kwa hakika hakuna. Mtu anapokuwa mwenye bidii utasikia kauli kama vile huyo hapendi mchezo, akishaingia kwenye kazi zake humpati, hageukagi nyuma kwenye kazi huyo, kama huyo yupo hiyo kazi lazima iishe, n.k.

Hizi ni baadhi ya kauli zinazoonyesha kuheshimiwa kwa mtu husika kutokana na kufanya kazi kwa bidii. Ikiwa unataka kuheshimika ni lazima ufanye kazi kwa bidii.

Ikiwa unafanya kazi kwa bidii huna haja ya kujikombakomba kwa wakubwa au mbele za watu ili utambulike; bidii yako ya kazi itakutambulisha.

Tunaamini umewahi kusikia watu wakipewa tuzo kwenye sherehe za kitaifa kutokana na kufanya kazi kwa bidii; hili linatupa picha ya kipekee ya faida ya kufanya kazi kwabidii.

Hivyo tunataka kuwatia moyo wajasiriamali popote pale walipo na wahakikishe wanapambana kwa nguvu zote ili kujikomboa na kuhakikisha wanaachana na dhana ya uvivu.




## FIKRA YA MJASIRIAMALI

### Mambo mawili kabla hujaanza Kilimo

**UNAPOANZISHA mradi wa kilimo biashara, unatarajia mwisho wa siku uumalize kwa kupata faida, sasa basi leo nataka nikufahamishe mambo makubwa mawili unayotakiwa kuyajua kabla hujaanza mradi wako wowote wa kilimo.**

Unapoanzisha mradi unatarajia mwisho wa siku uumalize kwa kupata faida, sasa basi leo nataka nikufahamishe mambo makubwa mawili unayotakiwa kuyajua kabla hujaanza mradi wako wowote wa kilimo.

Katika kilimo biashara, hili ni jambo la kwanza na muhimu sana kulifahamu. Farming master-plan ni muongozo wa shughuri zote unazotakiwa kuzifanya katika kilimo chako tangu kuandaa shamba mpaka kuvuna.

Hii ijumuishe shughuli kama kupanda, kudhibiti magugu, uwekaji wa mbolea na kupulizia madawa ya wadudu na magonjwa. Unatakiwa kujua shughuri hizi zote, muda wa kuzifanya, namna ya kuzifanya na mahitaji yake ili uzifanye.

Kwa mfano uwekaji wa mbolea: wakati gani uweke kiasi gani, uwekeje? Unatakiwa ufahamu haya yote kabla hujaanza mradi wako wa kilimo ilii usipate usumbufu wakati wa utekelezaji.

Jambo la pili: Makadirio ya Gharama za Uzalishaji na faida

Hili ni jambo lingine muhimu sana. Naamini unapofanya kilimo biashara hujaamua kulima ili ujifurahishe tu, unalima ili upate faida. Hivyo basi unatakiwa ujue mradi wako utakugharimu kiasi gani katika utekelezaji wake na mwisho wa siku utakulipa kiasi gani? Pengine hutopata gharama halisi lakini ni lazima ufahamuu japo makadirio ya gharama ili kwanza uweze kujipanga lakini pia usikwame katika utekelezaji wa mradi wako.

Kwanini ni muhimu kufahamu mambo haya? Utajua mahitaji muhimu unayotakiwa kuwa nayo kabla hujauanza mradi wa kilimo. Utapata fursa ya kuona mradi wako katika hatua mbalimbali hata kabla hujauanzisha. Utaweza kujua makadirio ya gharama za uzalishaji na faida tarajiwa

Kwa hiyo nikunasihi ndugu yangu usianzishe mradi wako wa kilimo mpaka ujiridhishe kuwa una ufahamu wa mambo haya mawili.

# Vuta watalii Mtandaoni, ila zingatia hili

**VITU vya kuzingatia unapofanya biashara mtandaoni Tanzania ni muhimu kufahau mapema kwasababu Kufanya biashara kwenye mtandao ni jambo lenye faida na changamoto zake.**

Unaweza ukawa na bidhaa nzuri sana lakini ukumbuke kuwa kila siku kunaanzishwa tovuti za kuuza bidhaa mtandaoni.

Haijalishi kuwa wewe ni muuzaji wa bidhaa wa siku nyingi au wa karibuni, ni wazi kuwa utakutana na changamoto kadha wa kadha.

**Jitahidi Kukosa Wateja**

Ni rahisi mtu kukaa dukani kwake siku nzima ili kuwahudumia wateja; lakini unaona hakuna umuhimu wa kukaa karibu na wateja wake wa kwenye mtandao.

Kumbuka hawa ni wateja kama wateja wengine, wanaweza kuwa wana maswali, maombi au mapendekezo wanayotaka kuyafikisha kwako.

Wateja watakufikia vipi na wewe hujaweka mfumo mzuri wa huduma kwa wateja? Je watanunua tu vitu kwa sababu unapenda wanunue? La hasha! Kutokana na kosa hili hutoweza kupata wateja na kufanikiwa katika biashara yako.

Epuka Kutengeneza Website Mbaya

Katika jambo muhimu kwenye biashara ya kwenye mtandao ni tovuti iliyotengenezwa au kusanifiwa vizuri. Watu wengi hutengeneza tovuti mbaya ambazo siyo rafiki kwa wateja na vifaa vyao.

Hili huwagharimu wengi kwa kupoteza wateja wengi. Zingatia mambo haya katika kutengeneza tovuti nzuri ya kufanyia biashara ya kwenye mtandao:

Hakikisha inaweza kuonekana vyema kwenye vifaa vyote kama vile simu, tablet na kompyuta.

Hakikisha ina mfumo mzuri wa viungo (Menu and Navigation) kwa njiaa hii mteja ataweza kuperuzi vyema kwenye tovuti yako. Hakikisha inasehemu ya utafutaji.

Ukizingatia mambo haya tovuti yako itakuwa nzuri kwa wateja na kukufanya kupata mauzo zaidi.

**Epuka Ufafanuzi Mbovu wa Bidhaa**

Hakuna mtu anayenunua kitu ambacho hajakifahamu vizuri au kukiona. Kosa la ufafanuzi au maelezo duni ya bidhaa limewafanya wateja wengi kutonunua bidhaa za wafanya biashara wengi.

Hakikisha bidhaa ina picha nzuri na maelezo ya kutosha kumfanya mteja aielewe bidhaa yako ili awe tayari kuinunua.

Kwa mfano mtu unaweka picha ya bidhaa fulani kwenye tovuti au mtandao wa kijamii bila hata maelezo yoyote, je unafikiri kwa sababu umeiweka kama cover au profile picture ndiyo itanunuliwa? Ni lazima watu wapate maelezo ya kutosha na jinsi bidhaa husika itakavyowasaidia ndipo watainunua.

Jitahidi Kutumia Mitandao Ya Kijamii

Wafanya biashara wengi hawajui umuhimu wa mitandao ya kijamii wala matumizi yake kwenye biashara zao.

Biashara ya kwenye mtandao inahitaji ufahamu matumizi mazuri ya mitandao ya kijamii ili kupata wateja wengi zaidi kwa ajili ya bidhaa zako.

Hakikisha unawajulisha watu jinsi bidhaa zako zitakavyotatua matatizo yao pia usisahau kuwajulisha punguzo (offer), bei na njia ya kuzipata bidhaa zako.

**Epuka Kutokufahamu Wateja, Soko Lako**

Kufahamu wateja na soko ni hatua mojawapo ya kukuwezesha kukuza mauzo ya bidhaa zako.

Hebu fikiri unatangaza bidhaa za urembo za wanawake kwenye group la wa Whatsapp, je utapata wateja kweli? Naamini hutopata wateja jinsi ipasavyo.

Ni wazi kuwa ni muhimu ujue soko lako liko wapi na ulilenge ipasaavyo.

Epuka Mfumo Mbovu wa Kulipia Bidhaa

Mara nyingi unapouza vitu kupitia mtandao wateja watalipia bidhaa zao moja kwa moja, pia watafahamu jisi watakavyopata bidhaa husika.

Wauzaji wengi hawaweki mfumo rahisi kwa wateja ili waweze kufanya malipo kwamfano tovuti za Afrika Mashariki tunategemea kuona njia za malipo kwa njia za mtandao.

Pia ni lazima kuwe na mfumo mzuri wa kuwasafirishia au kuwafikishia wateja bidhaa zao. Kwa kufanya hivi utaaminika zaidi na kujiongezea wateja

Jitahidi Kutatua Matatizo Kuliko Kuuza Bidhaa

Mara nyingi nimekuwa nikisisitiza kuwa pesa ni matokeo ya kutatua shida za watu.

Pamoja na kulenga kuuza bidhaa zako na kupata pesa, ni lazima kwanza uhakikishe unatatua matatizo ya watu kupitia bidhaa zako kwanza.

Ni muhimu pia kujenga imani kwa wateja kwa kuwapa garantii na punguzo (offer) kwa ajili ya bidhaa zako.

Kwa kufanya hivi utaongeza imani ya watu kwenye bidhaa na biashara yako.

**Jitahidi Kujitangaza Zaidi**

Biashara ni matangazo Jinsi matangazo yalivyo muhimu katika biashara za aina nyingine, ndivyo ilivyo pia kwenye biashara ya kwenye mtandao.

Ni lazima utumie njia mbalimbali za kuzitangaza bidhaa zako, ukihusisha njia za bure na zile zakulipiwa.

Kwa njiaa hii utawezakutambulika kati ya washindani wako, hivyo kufikia wateja wengi zaidi.

Kamwe usifanye kosa la kuupuuzia matangazo kwenye biashara ya kwenye mtandao kwani kuna ushindani mkubwa.





# Njiwa si uchawi, fuga utoboe

NA MWANDISHI MAALUM

**UFUGAJI wa njiwa ni shughuli inayoongezeka nchini Tanzania ikichangia katika kutoa chakula, ajira na kipato kwa familia nyingi, ingawa katika baadhi ya jamii wanaona kama kuna ushirikina ndani yake, hii si kweli.**

Njiwa ni ndege wanaojulikana kwa uzuri wao na sauti zao nzuri, lakini pia wanatoa bidhaa muhimu kama vile mayai na nyama.

Katika mwongo huu, tutachambua kwa kina faida za ufugaji wa njiwa, mbinu bora za kufuga, changamoto zinazoweza kujitokeza, na mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo.

**1. Maelezo ya Msingi Kuhusu Njiwa**

Njiwa ni ndege wa familia ya Columbidae, na kuna aina nyingi zinazopatikana. Aina maarufu zinazofugwa nchini Tanzania ni pamoja na:

Njiwa wa Kienyeji: Hawa ni njiwa wadogo wenye uwezo wa kuishi katika mazingira mbalimbali. Wanaweza kuishi kwenye mazingira ya miji na vijiji, na wanajulikana kwa uwezo wao wa kuzaa mayai mengi.

Njiwa wa Kisasa: Hizi ni aina za njiwa zinazofugwa kibiashara ambazo zinaweza kutoa uzalishaji wa juu wa mayai na nyama. Njiwa hawa wanajulikana kwa ukuaji wao wa haraka na uzito mzuri.

**Faida za Ufugaji wa Njiwa Kibiashara**

Ufugaji wa njiwa unakuja na faida nyingi, ambazo ni pamoja na: Njiwa ni chanzo bora cha nyama yenye protini na mayai yenye virutubisho vingi. Nyama ya njiwa ina soko kubwa nchini, na mayai yao ni chakula bora chenye virutubisho vingi.

Urahisi wa Ufugaji

Njiwa ni rahisi kufuga ikilinganishwa na mifugo mingine kama ng'ombe na mbuzi. Wanaweza kufugwa katika maeneo madogo, kama vile nyuma ya nyumba, bila haja ya eneo kubwa la ardhi.

Hii inawapa wafugaji fursa ya kujenga biashara bila kuhitaji mtaji mkubwa.

**Mchangiaji katika Usalama wa Chakula**

Ufugaji wa njiwa unachangia katika usalama wa chakula kwa kutoa chanzo kingine cha protini katika chakula cha jamii. Njiwa ni rahisi kukuzia, na wanaweza kuishi kwa chakula cha asili ambacho kinapatikana kirahisi.

Mafanikio ya Kiuchumi

Wafugaji wanaweza kupata kipato kizuri kupitia uuzaji wa nyama na mayai ya njiwa. Kuwepo kwa masoko mazuri kunawawezesha wafugaji kujenga biashara yenye faida na kuimarisha maisha yao.

**Mbinu Bora za Ufugaji wa Njiwa Kibiashara**

Ili kufanikisha malengo ya ufugaji wa njiwa, wafugaji wanapaswa kufuata mbinu bora za ufugaji. Hizi ni pamoja na banda la njiwa linapaswa kuwa na nafasi ya Kutosha: Kila njiwa anahitaji angalau mita za mraba 1-2. Banda linapaswa kuwa na nafasi ya kutosha kwa njiwa kuhamahama na kupumzika.

Wafugaji wanapaswa kuhakikisha banda lina ulinzi wa kutosha dhidi ya wanyama wa porini na wadudu.

Ventilasheni Bora: Kuwa na madirisha ya kutosha ili kuruhusu uingizaji hewa mzuri. Hii itasaidia kuzuia magonjwa yanayohusiana na upungufu wa hewa.

Usafi wa Kila Wakati: Usafi wa banda ni muhimu ili kuzuia magonjwa. Hakikisha unafanya usafi wa mara kwa mara kwa kuondoa mavi na uchafu.



Tumia madawa ya kuua vimelea na bakteria mara kwa mara.

Lishe ni muhimu katika kuongeza uzalishaji wa njiwa. Wafugaji wanapaswa kuzingatia yafuatayo:

Chakula cha Kitaalamu: Tumia chakula maalum cha njiwa ambacho kinajumuisha nafaka, majani, na virutubisho vingine muhimu. Chakula kinapaswa kuwa na kiwango cha juu cha protini, hasa katika kipindi cha ukuaji.

Maji Safi: Hakikisha njiwa wanapata maji safi kila wakati. Kila njiwa anahitaji angalau lita 0.5-1 za maji kwa siku. Maji yanapaswa kubadilishwa mara kwa mara ili kuhakikisha usafi.

Ratiba ya Lishe: Kuwa na ratiba ya lishe ambayo inahusisha chakula cha majani, nafaka, na virutubisho vingine. Ratiba hii inaweza kubadilishwa kulingana na umri na uzito wa njiwa.

**Huduma za Afya**

Huduma bora za afya ni muhimu ili kuzuia magonjwa na kuhakikisha njiwa wanabaki na afya nzuri.

Wafugaji wanapaswa kuzingatia yafuatayo:

Chanjo: Kutoa chanjo dhidi ya magonjwa kama vile Newcastle Disease na magonjwa mengine ya kawaida ya njiwa.

Ufuatiliaji wa Afya: Fuatilia afya ya njiwa kila siku kwa kuangalia dalili za magonjwa kama vile kikohozi, homa, au upotevu wa hamu ya kula. Ni muhimu kutoa matibabu mara moja wanapokutana na dalili hizi.

Udhibiti wa Vimelea: Tumiza dawa za kuzuia vimelea kama minyoo na kupe. Hii itasaidia kuzuia kuenea kwa magonjwa na kuimarisha uzalishaji wa njiwa.

**Mafunzo na Uelewa wa Ufugaji**

Wafugaji wanapaswa kuendelea kujifunza kuhusu mbinu bora za ufugaji kupitia mafunzo na warsha zinazotolewa na wataalamu.

Hii itawasaidia kuboresha ujuzi wao na kuongeza uzalishaji. Pia, ni muhimu kushirikiana na wataalamu wa mifugo ili kupata ushauri na msaada.

Ingawa ufugaji wa njiwa una faida nyingi, kuna changamoto kadhaa: Magonjwa yanaweza kuathiri uzalishaji na afya ya njiwa.

Hii inahitaji wafugaji kuwa makini katika ufuatiliaji wa afya. Magonjwa kama vile Newcastle Disease yanaweza kuleta madhara makubwa. Gharama za chakula zinaweza kuathiri faida ya mfugaji.

Bei ya chakula inaweza kuathiriwa na hali ya hewa, ugonjwa wa mimea, na uzalishaji wa mazao. Wafugaji wanapaswa kuandaa bajeti na mipango ya kukabiliana na ongezeko la gharama.

# Kinachotukia Goma, Dunia imejiroga wapi?

**INASIKITISHA sana kwa kile kinachoendelea ndani ya Goma mji wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kwa sasa hakuna kinachoendelea zaidi ya risasi na mabomu tu. Dunia imekaa inatazama, nini kinachotukia.**



Je, ni ubinafsi, choyo, tamaa au ulimbukeni? Damu ya watoto wasio na hatia ipo mikononi mwa watu wenye kutaka kufanikisha mambo yao. Ni kilio kitupu.

Wakati mapambano yanaendelea, sasa wataalam wa Umoja wa Mataifa wanatoa uhakikisho kuwa Jeshi la Rwanda linaongoza operesheni za M23, wakielezea jinsi makurutu wa M23 wanavyopewa mafunzo chini ya usimamizi wa Rwanda na kupewa silaha za hali ya juu za nchi hiyo.

Mji wa Goma uko karibu na Ziwa Kivu kwenye mpaka na Rwanda. Huu ni mji mkuu wa Jimbo la Kivu Kaskazini lenye utajiri wa madini na ni kitovu muhimu cha biashara, kituo cha kutoa huduma ya kibinadamu na kituo cha ujumbe mkubwa zaidi wa kulinda amani wa Umoja wa Mataifa.

Jiji hilo pia lilikuwa kimbilio la wale wanaokimbia mzozo kati ya wapiganaji wa M23 na jeshi ambao ulizuka tena mwishoni mwa 2021 na idadi ya watu ikiongezeka hadi karibu milioni mbili.

Wakazi wa jiji hilo wanakabiliwa na hatari zaidi baada ya mapigano kuzuka tena Jumapili usiku. Makabiliano makali yaliyoshuhudiwa yamesababisha maafa yaliyoacha miili ya watu ikiwa imetapakaa mitaani. Hali halisi ya kinachoendelea haijulikani kwasababu mawasiliano ya simu, huduma za umeme na usambazaji wa maji pia imekatizwa. Lakini M23 wanasadikiwa kuteka sehemu kubwa ya jiji hilo.

"Suala la iwapo wanajeshi wa Rwanda kuunga mkono wapiganaji wa M23 ndani ya Goma halina mjadala ," alisema mkuu wa kikosi cha kulinda amani cha Umoja wa Mataifa Jean-Pierre Lacroix, japo aliongeza kuwa ilikuwa vigumu kutaja idadi kamili katika eneo la Goma.

Jumatatu wiki hii baadhi ya wanajeshi wa jeshi la Congo waliokuwa Goma walijisalimisha kwa kuvuka mpaka na kuingia Rwanda.

Tangu mzozo huo uanze, Rais Kagame mara kwa mara amekanusha kuhusika kwa namna yoyote katika kusaidia waasi wa M23, ambao wana vifaa vya kutosha, silaha za kutosha na mafunzo ya kutosha.

Hata hivyo, msimamo huo umebadilika sana huku shutuma zikiendelea kuongezeka huku 'uwezo mkubwa' wa kundi hilo la waasi ukioonyesha uungaji mkono wa Rwanda, kulingana na Richard Moncrief, mkurugenzi wa mradi wa International Crisis Group kwa Maziwa Makuu.

Siku ya Jumapili, Wizara ya Mambo ya Nje ya Rwanda ilisema katika taarifa yake: "Mapigano yanayoendelea karibu na mpaka wa Rwanda ni tishio kwa usalama wa Rwanda, na hivyo basi Rwanda haina budi kujilinda."

Ilisema inasikitishwa na kauli za "kupotosha na za kijanja" zisizo na msingi zinazotolewa kuhusu mzozo huo.

Kwa Kagame, muktadha wa yote haya unatokana na mauaji ya halaiki ya Rwanda ambayo yalifanyika kwa siku 100 mwaka 1994.

Wanamgambo wa kabila la Wahutu waliohusika na mauaji ya hadi watu 800,000 wengi wao kutoka jamii ya Watutsi walikimbilia eneo ambalo sasa ni DR Congo, wengine wakijiunga na Democratic Forces for the Liberation of Rwanda (FDLR).

Kundi hili la waasi bado linafanya kazi katika eneo la mashariki mwa DR Congo ambalo halijatulia - na bado linajumuisha baadhi ya wale waliohusika na mauaji ya halaiki.



Kagame, ambaye aliongoza kikosi cha waasi cha Watutsi ambacho kilimaliza mauaji zaidi ya miongo mitatu iliyopita, anawachukulia "wanamgambo hao wa mauaji ya halaiki" kama tishio lililopo.

Serikali ya Kagame imevamia Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo mara mbili, ikisema inataka kuzuia vikundi vya waasi wa Kihutu kufanya mashambulizi ya kuvuka mpaka.

Mapema Mwezi huu, alimshutumu Rais wa DR Congo, Félix Tshisekedi, kwa kushindwa kushughulikia FDLR na kuzungumza na M23, akisema kuwa hili linazidi kuzidisha mgogoro.

Moncrief anaamini kuwa shambulizi la Goma linahusiana zaidi na kutoa ujumbe wa kisiasa, akisema kuwa M23 halihitaji jiji hilo kimkakati kwani tayari "linadhibiti maeneo mengi yenye faida zaidi."

"Ni njia ya Rais Kagame kuonyesha nguvu yake juu ya nani anayeongoza Kivu Kaskazini," alisema mtaalamu wa Maziwa Makuu.

Rwanda ilimlaumu gavana wa kijeshi wa Kivu Kaskazini, ambaye aliuawa katika mapigano wiki iliyopita, kwa kushirikiana na FDLR.

Wataalamu wanakubaliana kuwa kugundulika kwa ushirikiano wa kiwango cha juu kama huu, ingekuwa kama changamoto kuu kwa Rwanda.

Asili ya M23 inahusishwa na mivutano hii ni kundi la waasi ambalo linasema linapigania maslahi ya jamii ya Watutsi walio wachache mashariki mwa DR Congo.

Uasi wake wa kwanza wa zaidi ya muongo mmoja uliopita ulimalizika kwa makubaliano ya amani - wapiganaji wake walipokonywa silaha na wengi wao wakahamia katika kambi nchini Uganda.

Lakini miaka mitatu iliyopita, walianza kuondoka kambini wakisema mpango wa amani haukuheshimiwa na ndani ya miezi michache wakaanza kuteka maeneo.

Ujumbe wa kulinda amani wa Umoja wa Mataifa - uliotumwa mara ya kwanza mwaka 1999 - hauna mamlaka ya kufanya mashambulizi. Vikosi viwili vya kikanda - kimoja cha Afrika Mashariki kikifuatiwa na cha kusini mwa Afrika - vilitumwa miaka michache iliyopita kwa ombi la Tshisekedi, lakini vimeshindwa kuwadhibiti M23.

Kulingana na kundi la wataalamu wa Umoja wa Mataifa, uwezo wao unajumuisha mafunzo ya miezi mitano katika kambi kuu ya M23 huko Tchanzu, eneo lenye milima, si mbali na mpaka wa Rwanda. Mafunzo hayo yanajumuisha kozi za nadharia na itikadi na kisha vitendo ikiwa ni pamoja na "mbinu za vita," "sheria za mapambano" na "mbinu za msituni."

Inaelezwa kuwa maafisa wa Rwanda mara nyingi walikuwepo kwenye kambi hiyo, ambapo waajiriwa, wakiwemo watoto, waliletwa - wengine wakijiunga kwa hiari, wengine walilazimishwa kujiunga kupitia operesheni maalumu ambapo machifu wanalazimika kutoa wapiganaji.

Wataalamu hao walisema Sultani Makenga, aliyepigana upande wa Kagame mwanzoni mwa miaka ya 1990 nchini Rwanda na sasa ni mkuu wa waasi wa M23, alihudhuria baadhi ya sherehe za waliofariki dunia kati file:///C:/Users/WANANCHI%20SPOTI/Desktop/20250201_MAP005.webp ya Septemba 25 na 31 Oktoba 2024 zilizohusisha wapiganaji 3,000.

Msemaji wa serikali ya Rwanda, Yolande Makolo hakujibu swali la iwapo maafisa wa Rwanda walikuwa katika kambi ya M23 au la, lakini alikanusha tuhuma kuhusu askari watoto.

Hata hivyo wataalamu wa Umoja wa Mataifa wanaeleza jinsi nguvu za M23 zilivyoongezeka tangu mwezi Mei, wakati huo ilipokuwa na wapiganaji karibu 3,000.

Wataalamu hao wanakadiria kuwa kati ya wanajeshi 3,000 na 4,000 wa jeshi la Rwanda wako ardhini nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo - wakisema idadi hiyo inatokana na uthibitisho wa picha, picha za ndege zisizo na rubani, rekodi za video, ushuhuda na ujasusi.

Wapiganaji waliokamatwa wa M23 walisema kuwa Wanyarwanda wanajulikana kuwa ni 'friendly force' (vikosi rafiki,) na ripoti ya wataalamu ya mwezi Disemba inasema neno hilo la Kiingereza "lilitumiwa na wote" hata wakati ambao waliohojiwa walipokuwa wakizungumza kwa lugha zingine.

Walisema vikosi hivi maalumu vya Rwanda vilikuwepo huko kutoa mafunzo na kuwasaidia waasi, na hawakuingiliana na wapiganaji wa kawaida wa M23.

Mshirika wa Rwanda, Uganda, ambaye anapambana na kundi jingine la waasi nchini DR Congo ambalo linatishia usalama wake, pia inashutumiwa kuwasaidia M23 - huku maafisa wake pia wakionekana Tchanzu.

Wataalamu hao wa Umoja wa Mataifa wanasema Uganda pia imesambaza silaha, kuwakaribisha viongozi wa waasi na kuruhusu shughuli za kuvuka mpaka za wapiganaji wa M23 shutuma ambazo Kampala inazikanusha.

Hivi karibuni Kagame alieleza kusikitishwa kwake, kwamba baada ya Tshisekedi kuingia madarakani mwaka 2019, pendekezo la Rwanda la kushirikiana na jeshi la Congo kukabiliana na FDLR lilikataliwa. Ni tofauti na mashambulizi ya pamoja ya DR Congo na Uganda dhidi ya waasi wa Islamic Allied Democratic Forces (ADF).

Hilo linaweza kuelezea sababu ya kuibuka upya kwa M23 mwaka 2021 huku ushahidi unaonyesha uungaji mkono wa Rwanda kwa kundi hilo unaendelea kukua.

Wataalamu hao wa Umoja wa Mataifa wanasema uamuzi wa M23 wa kuteka mji wenye madini wa Rubaya, ulioangukia mikononi mwa vikosi vyake mwezi Mei, "ulichochewa na hitaji la kimkakati la kuhodhi" biashara yenye faida kubwa ya madini ya coltan, ambayo yanatumika kutengenezea betri za magari ya umeme na simu.

Ripoti ya mwezi Disemba inasema kundi hilo sasa linakusanya takribani dola za kimarekani 800,000 (£643,000) kwa mwezi kutokana na ushuru wa coltan huko Rubaya - na kuhakikisha kwamba karibu tani 120 za madini hayo yanapelekwa moja kwa moja nchini Rwanda kila baada ya wiki nne.

Ripoti hiyo inajumuisha picha za satelaiti zinazoonyesha jinsi barabara ilivyopanuliwa kufikia mwezi Septemba katika upande wa Congo wa kivuko cha mpaka wa Kibumba, ili kuruhusu malori makubwa ambayo hapo awali hayakuweza kutumia njia hii ya kuingia Rwanda.

# Umuhimu wa Kuandaa Shamba



NA MWANDISHI WETU

**UDHIBITI wa Magugu: Kuandaa shamba mapema husaidia kudhibiti magugu kabla ya kupanda. Hii inatokana na kukatua udongo ambako huondoa na kuzika mbegu za magugu, hivyo kupunguza magugu ambayo yatatokea baadaye.**

Afya ya Udongo: Kwa kukatua udongo, masalia ya viumbe hai huchanganywa vizuri kwenye udongo, hivyo kuboresha muundo na rutuba ya udongo.

Udhibiti wa Wadudu: Kuandaa shamba mapema pia kusaidia kudhibiti wadudu kwa kuharibu mzunguko wa maisha yao na kupunguza idadi yao.

Wakati wa Kupanda: Kuandaa shamba mapema huhakikisha kwamba wakulima wanapanda mazao yao kwa wakati unaofaa, kitu ambacho ni muhimu sana ili kupata mavuno bora zaidi.

**Shughui za Kuandaa Shamba**

Maandalizi ya shamba yanahusisha mambo kadhaa ambayo yafaa kufanywa kabla ya msimu wa kupanda. Mambo hayo ni pamoja na:

Kupima Udongo: Vipimo vya udongo vitakusaidia kujua kiwango cha rutuba ya udongo, kiwango cha pH, na mambo mengine muhimu kwa ukuaji wa mazao.

Kukatua udongo: Kukatua udongo kutamega madongo yaliyoshikana, kuondoa magugu, na kuchanganya masalia ya viumbe hai.

Kuweka Mbolea: Weka mbolea kama samadi au mboji mapema ili kuupa udongo virutubisho muhimu kwa ukuaji bora wa mazao.

Umwagiliaji: Hakikisha kuna maji ya kutosha kwa ajili ya umwagiliaji na ikague mifumo ya umwagiliaji na kuirekebishwa kabla ya msimu wa kupanda.

Dhibiti Wadudu: Fuatilia idadi au kiwango cha wadudu na dhibiti au upunguze kabla ya msimu wa kupanda.

Mbegu ndio msingi wa kilimo. Na mavuno bora huanza na mbegu bora. Kwa mantiki hiyo ni muhimu sana kuchagua na kutumia mbegu bora mara zote unapotaka kulima.

**Chagua na panda mbegu bora**

Maandalizi ya mbegu ni mchakato muhimu unaohakikisha kuwa mbegu ni bora na ipo tayari kwa kupanda. Baadhi ya hatua muhimu katika maandalizi ya mbegu ni:

Uchaguzi wa Mbegu: Chagua mbegu bora ambazo zimetoka kwenye chanzo cha kuaminika kama vile mashirika ya serikali na sekta binafsi na ziwe zimeboreshwa kulingana na mazingira ya uzalishaji wa eneo husika.

Usafishaji wa Mbegu: Mbegu zinapaswa kusafishwa ili kuondoa uchafu, mbegu mbovu au zenye magonjwa. Hii itahakikisha kuwa unabaki na mbegu bora tu kwa ajili ya kupanda.

Kutibu Mbegu kwa viuadudu: Mbegu zichanganywe na dawa za kukinga dhidi ya fangasi, bakteria, virusi au wadudu na magonjwa mengine.

Pima uotaji wake: Mbegu zinapaswa kupimwa kujua uotaji na ustawi wake ili kuhakikisha kuwa zitakua vizuri baada ya kupanda.

Mbegu bora ni mbegu ambazo ama zimezalishwa nchini au zimeletwa nchini kutoka nje ya nchi na kisha zikathibitishwa na mamlaka ya kudhibiti ubora wa mbegu nchini Tanzania, TOSCI.

Mbegu bora zinaweza kuzalishwa kutoka kwenye vituo vya utafiti wa kilimo vya serikali (TARI) au makampuni binafsi. Mbegu zinazozalishwa na vituo vya utafiti vya serikali zinasambazwa na kuuzwa na Wakala wa Mbegu za Kilimo nchini, ASA.

**Mbegu bora zina sifa zipi?**

Ili ujue kama mbegu husika ni bora au la, angalia sifa zifuatazo: Usafi. Mbegu bora inatakiwa kuwa safi bila taka taka zozote wala mbegu mbovu.

Aina moja tu. Mbegu bora haitakiwa kuwa imechanganyika na mbegu nyingine yoyote hata kama ni ya zao moja. Mbegu zote zinatakiwa zifanane rangi, muundo, na ukubwa.

Kuthibitishwa na TOSCI. Mbegu zote zinazotumika Tanzania ni lazima ziwe zimethibitishwa na ziwe na stika ya TOSCI.

Uotaji mzuri. Mbegu ni lazima iwe na uwezo mzuri wa kuota, angalau asilimia 90.

Zinazaa sana: Mbegu bora zina uwezo mkubwa wa kuzaa kuliko mbegu za kienyeji, kitu ambacho kitaongeza wingi wa mavuno.

Hukomaa kwa muda mfupi sana: Kuna baadhi ya mbegu za kisasa zinakuchukua mpaka siku 60 tangu kupanda mpaka kuvuna.

Zinavumilia dhidi ya Magonjwa na wadudu: Mbegu bora haziathiriwi sana na magonjwa na wadudu hivyo kupunguza gharama za kutumia viuatilifu.

Zinaendana na Mazingira: Mbegu bora zina uwezo mkubwa wa kuendana na hali za kimazingira kwa kuwa zimezalishwa na kujaribiwa katika maeneo husika.

Zinakua kwa usawa: Mbegu bora zinaachipua na kukua kwa usawa zaidi, na kusababisha mazao kustawi vizuri na kwa usawa.



# Kilimo cha vitunguu saumu vitakavyokutoa

NA MWANDISHI WETU

**KILIMO cha vitunguu saumu nchini Tanzania kinapata umaarufu kwa kasi kama biashara ya kilimo yenye matumaini, kutokana na ongezeko kubwa la mahitaji ya ndani na katika soko la kimataifa.**

Vitunguu saumu, kwa harufu na ladha yake kali na ya kipekee, uwezo wake kitiba, na kutumika kwake katika matumizi mbalimbali ya mapishi, vimejipatia nafasi muhimu katika majiko ya kaya nyingi za Kitanzania. Umaarufu wake haujaja tu kwa bahati, bali ni ushahidi wa matumizi yake lukuki na faida zake nyingi za kiafya.

Hali mbalimbali za hewa na udongo wenye rutuba nchini Tanzania hutoa mazingira bora kwa kilimo cha vitunguu saumu. Kuanzia milima ya kijani ya Arusha na Kilimanjaro hadi tambarare za Morogoro na Singida, maeneo mbalimbali ya kijiografia ya nchi yetu yanachangia katika ukuaji wa zao hili muhimu.

Kila eneo lina faida za kipekee; iwe ni baridi kali la milimani linalonenepesha punje na kuzipa ladha yake ya ukali au udongo wenye rutuba usiotuamisha maji unaostawisha na kuleta tija kwenye vitunguu saumu.

Kwenye makala hii, tutaangalia mambo muhimu kwenye kilimo cha vitunguu saumu nchini Tanzania, na kutoa mwongozo kamili kwa wakulima wenye uzoefu na wale wapya kwenye uwanja huu. Tutazidadavua mada muhimu kama vile kuchagua aina za vitunguu saumu zinazofaa kwa eneo lako, kutekeleza mbinu bora za kilimo, na kugusia mienendo ya soko la vitunguu saumu.

Ukielewa misingi hii, utakuwa na maarifa ya kutosha kufanikiwa katika kilimo cha vitunguu saumu, kukidhi mahitaji ya soko, na hatimaye kuchangia kwenye ukuaji wa sekta ya vitunguu saumu nchini.

Uwe mkulima mzoefu anayetaka kuangazia fursa kwenye mazao mengine au mkulima mpya anayetaka kuanza safari ya kilimo, kitabu hiki kinalenga kukupa maarifa ya msingi na mwongozo wa vitendo utakaohitaji ili kufanikiwa katika kilimo cha vitunguu saumu.

Ambatana nasi tunapoibua fursa na changamoto kwenye kilimo hiki, na uone jinsi utakavyoweza kuifanya kuwa biashara yenye faida na mafanikio.

**Hali ya hewa na maji au mvua**

Vitunguu saumu vinapendelea hali ya joto la kati ya nyuzi 12 – 24 za sentigredi. Wastani wa mm 500 – 600 za mvua zinatosha kwa msimu wote wa uzalishaji.

Unyevu anga na au mvua nyingi sana huvutia magonjwa ya ukungu. Kwa mantiki hii vitunguu saumu vinafaa zaidi kulimwa katika maeneo yoyote ambayo yanamvua chache na uhakika wa maji ya kumwagilia.

**Udongo na Mwinuko**

Vitunguu saumu hupendelea udongo wenye rutuba usiotuamisha maji na wenye pH ya kati ya 5.5 – 7.5. Vitunguu saumu vinapendelea maeneo yenye miinuko ya kati ya mita 1000 hadi 2500 kutoka usawa wa bahari.

Udongo wa tifutifu kichanga (sandy loam) unafaa zaidi kwa vitunguu saumu kwa kuwa unapitisha hewa vizuri na hautuamishi maji. Udongo wa mfinyanzi mzito hauruhusu vitunguu kujitanua na hutunza maji kwa muda mrefu sana hivyo kuozesha vitunguu.

**Mikoa inayolima vitunguu saumu Tanzania**

Kwa hapa Tanzania vitunguu saumu vinalimwa zaidi katika mikoa ya Mbeya, Iringa, Manyara, Arusha, na Kilimanjaro. Mikoa mingine ni Morogoro (Mgeta) na Singida.

Maeneo ya nyanda za juu yana miinuko stahiki , hali ya hewa ya baridi na mtawanyiko mzuri wa mvua (vitu) ambavyo huchagiza sana ustawi wa vitunguu saumu hasa vya hardneck.

Tuna Mwongozo wa kilimo biashara wa zao hili, kwanini usiupate ili upate maelezo mengi yenye kina zaidi?

Kwenye mwongozo utapata mapendekezo maalum kutoka kwetu juu ya aina bora na kiasi sahihi cha mbegu, mbolea na viuatilifu. Pamoja na uchambuzi wa gharama za uzalishaji katika kila hatua na faida utakayopata.



Vitunguu saumu vipo vya aina mbili: Vitunguu saumu vya shingo laini (soft-neck garlic) na Vitunguu saumu vya shingo ngumu (hard-neck garlic). Aina hizi zote zinalimwa hapa nchini.

**Vitunguu saumu vya shingo laini (Soft-neck Garlic)**

Hivi ni vitunguu saumu ambavyo shina lake au shingo yake ni laini na ina tabia ya kuanguka (au kulala) vitunguu vinapokomaa. Shina la vitunguu hivi huwa ni laini hata baada ya vitunguu kuvunwa na inaweza kusokotwa kama kamba. Dalili ya kukomaa vitunguu hivi ni kulala au kuanguka kwa shina lake.

Mfano wa vitunguu saumu vya shingo laini ni Egyptian white garlic na Chinese white garlic. Sifa za vitunguu saumu vya shingo laini

Shingo yake ni laini kiasi kwamba inaweza kukunjwa au kusokotwa kama kamba. Vina punje (cloves) ndogondogo nyingi (12 – 25) zilizopangwa katika safu nyingi ndani ya tunguu (bulb). Kutokana na uwingi wa punje, matunguu (bulbs) yake ni makubwa kuliko ya hardneck.

Vina ladha na harufu yenye ukali wa wastani, inayofaa kwa matumizi ya kawaida ya nyumbani. Ladha yake ni laini kuliko ile ya vitunguu saumu vya shingo ngumu.

Ni rahisi kulima na vinahifadhika kwa muda mrefu zaidi: kati ya miezi 10 hadi 12. Vinastawi katika maeneo yenye hali za hewa mbalimbali, kuanzia baridi hadi joto la wastani, na vinaweza kupandwa katika maeneo ya kitropiki na uwanda wa kati.

Vitunguu saumu vya shingo ngumu (Hard-neck Garlic)

Hivi ni vitunguu ambavyo shina lake (au shingo yake) ni ngumu kama mti na hubakia imesima hata vitunguu saumu vinapokomaa. Dalili ya kukomaa kwa aina hii ni majani kubadilika rangi kuwa kahawia na kuanza kukauka.

Sifa za vitunguu saumu vya shingo ngumu

Vitunguu saumu vya hardneck hutoa shina linaloitwa scape. Shina hilo linaanzia kwenye kitako cha kitunguu na kupanda hadi kwenye shingo, na hivyo kuvipa jina la "hard-neck – shingo ngumu". Shingo yake ni ngumu na hubaki imesimama kama mti, na hutoa maua kwa juu.

Vina punje (cloves) chache kubwa (4 – 12) zilizopangwa katika mduara mmoja ndani ya tunguu (bulb) kuzunguka shingo ngumu (scape). Matunguu yake ni madogo kuliko ya softneck.

Vina ladha na harufu kali zaidi inayopendwa na wapishi wengi.

Ni vigumu kulima na vinahifadhika kwa muda mfupi zaidi: kati ya miezi 4 hadi 8.

Vinapendelea zaidi katika maeneo yenye baridi kali, na hivyo kustawi vizuri zaidi maeneo ya nyanda za juu. Hali hii ya baridi ndio hufanya vitengeneze punje (cloves) nene zenye ladha na harufu kali.

# Faida za Kufanya Biashara Kwa Bidii

**KUNA fikra potofu zimejengeka miongoni mwa watu wakidhani kuwa kufanya kazi kwa bidii ni utumwa. Hii ni kutokana na dunia ya sasa kujaa watu wasiopenda kazi na wavivu.**

**1. Bidii inasaidia Kutumia Muda Vyema**

Huwezi kutumia muda vyema kama hutofanya kazi kwa bidii. Ukiwa na bidii katika kufanya kazi, unaweza kufanya kazi za siku nzima ndani ya saa moja au kazi za siku mbili ndani ya siku moja.

Hakuna mtu yeyote aliyefanikiwa bila kutumia muda vyema; muda ni mali, hivyo yakupasa uutumie vyema kwa kufanya kazi kwa bidii.

**2. Bidii inasaidia Kufikia Malengo Yako**

Kanuni moja wapo ya kufikia malengo ni kufanya kazi kwa bidii. Safari ya mafanikio siyo ya mteremko, inahitaji juhudi nyingi ili tuweze kuona matokeo.

Hakuna mtu aliyewahi kufanikiwa kwa kufanya kazi kivivu; fuatilia watu waliofanikiwa watakueleza jinsi wanavyofanya kazi usiku na mchana ili kukamilisha ndoto zao.

**3. Bidii inasaidia Kuheshimika**

Nani atamheshimu mvivu? Kwa hakika hakuna. Mtu anapokuwa mwenye bidii utasikia kauli kama vile huyo hapendi mchezo, akishaingia kwenye kazi zake humpati, hageukagi nyuma kwenye kazi huyo, kama huyo yupo hiyo kazi lazima iishe, n.k.

Hizi ni baadhi ya kauli zinazoonyesha kuheshimiwa kwa mtu husika kutokana na kufanya kazi kwa bidii. Ikiwa unataka kuheshimika ni lazima ufanye kazi kwa bidii.

**4. Bidii inasaidia Kutambulika**

Ikiwa unafanya kazi kwa bidii huna haja ya kujikombakomba kwa wakubwa au mbele za watu ili utambulike; bidii yako ya kazi itakutambulisha.

Naamini umewahi kusikia watu wakipewa tuzo kwenye sherehe za kitaifa kutokana na kufanya kazi kwa bidii; hili linatupa picha ya kipekee ya faida ya kufanya kazi kwabidii.

Usijali hata kama wanakudharau au wanakuona duni, wewe fanya kazi kwa bidii watakutambua ukiwepo au hata wakati utakapoondoka wataona pengo lako.

**5. Bidii inasaidia Kuondoa Lawama**

Mara nyingi idara au ofisi zenye malalamiko mengi ni zile zenye wafanyakazi wavivu. Pia wafanyakazi wengi wanaolaumiwa na kunyoshewa vidole na waajiri wao, wengi ni wale wavivu.

Ili kuepuka lawama au manung'uniko, ni vyema ukafanya kile unachokifanya kwa bidii kwani kwa njia hii utaongeza ufanisi wako.

**6. Bidii inasaidia Kupata Matokeo Makubwa**

Hakuna matokeo makubwa bila kazi kubwa, yaani kazi iliyofanywa kwa bidii. Kwa mtu yeyote anayetaka kuona matokeo makubwa katika kile anachokifanya ni lazima kwanza afanye bidii.

Kumbuka hata mkulima anayefanya bidii katika kilimo ndiye huvuna zaidi ya wakulima wengine. Hivyo kufanya kazi kwa bidii hakuepukiki kwenye maisha.

**7. Bidii inasaidia Huleta Fursa Mpya**

Mtu mwenye bidii kila mara hufungua milango ya kupata fursa mpya, kazi zake na bidii yake humtangaza na kumfungulia fursa zaidi. Hakuna mtu atakayempa mtu mvivu kazi au fursa zenye manufaa.

**8. Bidii inasaidia Kuboresha Afya**

Kukaa bila kufanya kazi ni kujiletea matatizo ya kiafya; kazi ni sehemu ya mazoezi. Hivyo kufanya kazi kwa bidii kutakufanya uwe mwenye afya njema kila wakati.

Unalotakiwa kukumbuka hapa ni kuwa na kiasi, fanya kazi kwa bidii lakini usipitilize hadi uathiri afya yako.





# Ili uwe Bilionea, fanya hivi

**KUNA wakati jarida maarufu la Forbes ilizua maoni mengi wakati lilipodai mmoja kati ya watu nyota kwenye mitandao ya kijamii kwa wakati huo, Kylie Jenner amepata utajiri wa karibu Dola bilioni 1.**

Haya ni mafanikio ambayo watu wachache sana wanaweza kuyapata na kulikuwa na watu 5,700 kote duniani waliokuwa na utajiri unaozidi dola milioni 500 2017 kulingana na ripoti kutoka kwa Global Wealth Report.

Mabilionea halisi hata hivyo ni wachache. Lakini mtu anahitaji nini hadi kuitwa bilionea?

## ANZISHA KAMPUNI

Ukiangalia watu matajiri duniani kwa mfano Jeff Bezos wa Amazon, Mark Zuckerberg wa Facebook, Amancio Ortega wa Zara na Jack Ma wa Alibaba ndio wanatawala.

Forbes inawatambua watu thuluthi mbili ya mabilionea 2,208 kuwa waliojizolea utajiri wao na idadi hiyo inazidi kuongezeka.

Kylie Jenner kumshinda Mark Zuckerberg kwa kasi ya utajiri

Ni kweli kuwa neno utajiri wa kujizolea linaweza kuwa na ugumu kulielezea. Hatua ya Forbes kumtaja Kylie Jenner ambaye alizaliwa katika familia tajiri kama aliyejipatia utajiri ilizua maoni mengi kwenye mtandao.

## PESA ZA URITHI

Karibu theluthi moja ya watu walio katika orodha ya Forbes walirithi pesa zao.

Hao ni pamoja na watu saba wa familia ya Walton, warithi wa maduka wa Walmart na Francoise Bettencourt-Meyers ambaye familia yake ilianzisha kampuni ya L'Oreal.

Mwanzilishi wa Amazon sasa ndiye mtu tajiri dunia. Urithi ni muhimu hasa barani Ulaya kutokana na kuwa umechangia kwa karibu nusu ya mabilionea kulinda na takwimu za Forbes za mwaka 2014.

Kuna sababu kadhaa zilizochangia watu ambao walirithi mali kuzidi kuongezeka.

Sababu moja ni kuwa thamani ya mali kama hisa imeongezeka kwa haraka kuliko mali nyingine miaka ya hivi karibuni.

## WEKEZA

Kuna zaidi ya watu 140 katika sekta ya fedha walio na utajiri unaozidi dola blioni 2.5 kwenye orodha ya watu matajiri.

Bill Gates alichukua tena uongozi wa kuwa mtu tajiri duniani na wengi wao ni kutoka nchini Marekani ambapo asilimia 25 ya mabilionea hupata utajiri wao kutoka sekta ya fedha.

Lakini usidhani kuwa ni rahisi kupata mafanikio hayo. Mkuu wa kampuni ya JP Morgan Chase boss Jamie Dimon ni baadhi ya mabilionea wachache waliochukua mkondo huo. Na wafadhili wengi karibu asilimia 20 ya watu matajiri zaidi ya 143 wana uhusiano na mifuko ya uwekezaji.

## HAMA ULIPO

Idadi ya mabilionea katika kila nchi inashuka, ila eneo linaloongezeka kwa watu matajiri duniani ni la Asia Pacific.

Karibu asilimia 29 ya watu mabilionea wapya mwaka uliopita walitokea eneo hilo kwa mujibu wa jarida la WealthX linalokadiria kuwa kuna mabilionea 2,750 duniani idadi iliyo juu kuliko ile ya Forbes.

China pekee ina mabilionea 29 kati ya 259 mabilionea wapya, idadi ya juu kuliko ya nchi yoyote.

Licha ya hatua zilizopigwa sehemu zingine duniani, Marekani inasalia nchi yenye mabilionea wengi zaidi ikiwa na mabilionea 585.

## USIWE MTU WA KESI

Mabilionea si wageni kwa kesi mahakamani. Kwa mfano Bill Gates, anaweza kujulikana kama mtu tajiri wa kutoa misaada lakini historia yake si safi vile.

Mnamo miaka ya tisini Marekani iliishtaki kampuni ya Microsoft kwa kutumia mbinu zinazozuia ushindani.

Serikali ya Marekani ilishinda na Microsoft ikakata rufaa. Kesi hiyo iliishia makubaliano. Tume ya Ulaya nayo ishaipiga faini kampuni ya Microsoft.

Baadhi ya kampuni ambazo pia zimepigwa faini ni pamoja na Google na Samsung na pia zile zisizo za teknolojia kama ya kamari ya Las Vegas Sands.



# Wachezaji waliowahi kunangwa na makocha wao

**KOCHA wa Manchester United, Ruben Amorim amegonga vichwa vya habari aliposema, ni bora kumuweka kama mchezaji wa akiba kocha wake wa makipa mwenye umri wa miaka 63, kuliko Marcus Rashford, kwa sababu hana juhudi.**



Rashford hajacheza kwenye kikosi cha United kwa muda wa wiki sita. Amorim anasema mshambuliaji huyo wa Uingereza hafanyi vyema katika mazoezi.

Mustakabali wake ndani ya Old Trafford haujulikani. Kuna klabu za Ulaya zinazohusishwa na kutaka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, kabla ya tarehe ya mwisho ya uhamisho wa wachezaji wiki ijayo.

Sio mara ya kwanza kwa kocha wa Ligi Kuu England kumkosoa hadharani mmoja wa wachezaji wake.

## Harry Redknapp na Darren Bent

Harry Redknapp alidai kuwa mke wake angefunga, pale Darren Bent alipokosa bao dakika za lala salama. Siku Tottenham ilipotoka sare ya 1-1 na Portsmouth Januari 2009.

Redknapp alisema: "Huwezi kupata nafasi nzuri zaidi ya kushinda goli kuliko ile uliyoipata. Hata mke wangu angeweza kufunga."

Licha ya kauli hiyo, Bent alibaki kwenye safu ya wachezaji wa Redknapp na alimaliza msimu wa 2008-09 kama mfungaji bora wa Tottenham akiwa na mabao 17, kabla ya kujiunga na Sunderland majira ya kiangazi.

Redknapp alitumia miaka mingine mitatu na nusu akiwa White Hart Lane (Tottenham) akiwasaidia kufika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa mwaka 2011, lakini alitimuliwa Juni 2012.

## Harry Redknapp na Adel Taarabt

Redknapp, wakati huo akiwa meneja wa QPR, hakusita kumkosoa Adel Taarabt alipoulizwa kwa nini kiungo huyo ameachwa nje ya kikosi kwenye mchezo dhidi ya Liverpool, Oktoba 2014.

"Siwezi kuwalinda watu ambao hawataki kukimbia na kufanya mazoezi, na wana uzito wa mawe matatu," alisema Redknapp.

"Alicheza katika mchezo wa timu ya kikosi cha pili juzi na ningeweza kukimbia zaidi ya alivyokimbia yeye. Siwezi kumchagua."

Taarabt ilijibu kwa kusema Redknapp alikuwa akitoa visingizio kutokana na matokeo mabaya ya timu hiyo, wakati huo timu ikiwa nafasi ya chini kwenye msimamo wa Ligi Kuu.

Kiungo huyo aliichezea klabu hiyo mechi tano tu, kabla ya kujiunga na Benfica msimu wa joto wa 2015.

QPR ilishuka daraja mwishoni mwa msimu wa 2014-15. Redknapp aliipandisha tena daraja timu hiyo msimu uliofuata kabla ya kung'atuka Januari 2015.

## Jose Mourinho na Luke Shaw

Jose Mourinho alimkosoa beki wa Uingereza, Luke Shaw wakati akiinoa Manchester United, akihoji kujitolea na utimamu wake.

Baada ya kuingia kama mchezaji wa akiba dhidi ya Everton Aprili 2017 Mourinho alisema beki huyo wa pembeni alitumia "mwili wake na ubongo wangu."

Aliongeza: "Alikuwa mbele yangu na nilikuwa nikimfanyia kila uamuzi."

Shaw bado yuko Old Trafford lakini ana jeraha, na amecheza mechi tatu tu msimu huu. Mourinho alifutwa kazi Disemba 2018 baada ya kuuanza vibaya msimu huo.

## Jose Mourinho na Tanguy Ndombele

Mourinho, alihamia Tottenham na kuwa meneja wa Tottenham, alimkosoa mchezaji aliyesajiliwa kwa pauni milioni 54, Tanguy Ndombele, Machi 2020.

Baada ya kiungo huyo kubadilishwa wakati wa mapumziko ya mchezo dhidi ya Burnley, Mourinho alisema: "Kipindi cha kwanza hatukuwa na safu ya kiungo. Yeye (Ndombele) amepata muda wa kutosha kupanda kiwango."

"Najua Ligi Kuu ni ngumu, na wachezaji wengine huchukua muda mrefu kuzoea ligi tofauti. Lakini mchezaji mwenye uwezo kama yeye, ni lazima atupe zaidi ya anachotupa sasa."

Hakukuwa na mwisho mwema kwa Mourinho wala Ndombele. Mourinho alitimuliwa Aprili 2021 baada ya kuiongoza kwa miezi 17, siku chache kabla ya fainali ya Kombe la Carabao dhidi ya Manchester City kwenye Uwanja wa Wembley.

Ndombele alipata tena nafasi katika timu wakati wa mechi za 2020-21, lakini alitumia misimu mitatu iliyofuata kwa mkopo kabla ya kuachiliwa kwa uhamisho wa bure Juni 2024.

## Pep Guardiola na Kalvin Phillips

Kocha wa Manchester City Pep Guardiola alidai Kalvin Phillips ni "mzito kupita kiasi" baada ya kurejea kutoka Kombe la Dunia la 2022 na ndio sababu iliyomfanya kuachwa nje ya kikosi kwa mechi ya raundi ya nne ya Kombe la Carabao dhidi ya Liverpool.

Phillips alisema maoni hayo "yaliharibu sana kujiamini kwake," huku Guardiola akiomba msamaha hadharani kwa kiungo huyo wa kati wa Uingereza.

Mchezaji huyo wa zamani wa Leeds aliichezea City mechi 27 kabla ya kujiunga na West Ham kwa mkopo Januari 2024. Kisha akahamia Ipswich kwa mkopo msimu uliopita.

## Erik ten Hag na Jadon Sancho

Kocha wa wakati huo wa Manchester United, Erik ten Hag hakumchezesha Jadon Sancho kwenye mechi dhidi ya Arsenal, Septemba 2023 kwa sababu aliamini winga huyo wa Uingereza hajafikia "kiwango" kinachohitajika mazoezini ili kujumuishwa.

Sancho alijibu kwa kusema, amefanywa "mbuzi wa kafara kwa muda mrefu."

Alilazimika kufanya mazoezi nje ya kikosi cha kwanza kabla ya kujiunga na klabu yake ya zamani ya Borussia Dortmund kwa mkopo mwezi Januari.

Ten Hag alifanya mazungumzo ya wazi na Sancho aliporejea United kutoka Borussia Dortmund, wakati wa mazoezi ya kujiandaa na msimu wa kiangazi mwaka 2024, lakini mchezaji huyo wa zamani wa Manchester City alijiunga na Chelsea kwa mkopo siku ya mwisho ya dirisha la uhamisho.

Ten Hag alifutwa kazi na Manchester United mwezi Oktoba huku klabu hiyo ikiwa nafasi ya 14 kwenye Ligi ya England, baada ya kushinda mechi tatu tu kati ya tisa za ufunguzi.

## Ange Postecoglou na Timo Werner

Kocha wa Tottenham, Ange Postecoglou alisema kiwango cha Timo Werner "hakikubaliki" baada ya kumtoa wakati wa mapumziko, katika mechi ya sare ya Ligi ya Europa dhidi ya Rangers mwezi Desemba.

"Tunahitaji kila mtu, akiwemo yeye kuchangia," alisema Postecoglou. "Nilitarajia kiwango kikubwa cha uchezaji kutoka kwa baadhi ya wachezaji waandamizi, na usiku wa leo haikuwa hivyo."

Mshambuliaji wa Ujerumani, Werner ameanza katika mechi mbili na mechi tano akitokea benchi tangu mchezo wa Rangers.

Postecoglou amesalia kwenye dimba la Tottenham lakini yuko chini ya shinikizo baada ya kufungwa mechi nane kati ya mechi 10 za Premier League.



# ARSENAL




## KWA OLLIE WATKINS

LONDON, England

**Arsenal wanatarajiwa kufanya jaribio la pili lilolo bora zaidi kumsajili mshambuliaji wa Aston Villa na England Ollie Watkins, 29, ambaye alikua shabiki wa Gunners.**





Nayo Manchester United wako kwenye mazungumzo ya muda na Barcelona kuhusu uhamisho wa mkopo wa mshambuliaji wa Uingereza Marcus Rashford, 27, lakini kuna wasiwasi wa iwapo klabu hiyo ya Uhispania itaweza kukamilisha dili kabla ya tarehe ya mwisho ya Jumatatu.

## MATHYS TEL ATAKIWA

LONDON, England

**ARSENAL wako tayari ku ipatia Bayern Munich ofa ya mshambuliaji wa Ufaransa chini ya umri wa miaka 21 Mathys Tel, 19, kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili la Januari.**



The Gunners na Chelsea wote wanachunguza uhamisho wa Tel, huku Manchester United pia wakifuatilia hali ya mchezaji huyo. Tottenham pia wana nia ya kumsaini Tel kwa mkopo mwezi huu.

## NAPOLI MBONA WAGUMU

MILAN, Italia

**NAPOLI wamekataa dau la euro 65m (£54.5m) kutoka kwa Galatasaray kufanya uhamisho wa mkopo wa mshambuliaji wa Nigeria Victor Osimhen, 26, kuwa wa kudumu.**



Newcastle United wanatazamiwa kuzishinda klabu kadhaa za Premier League kumsajili winga wa kimataifa wa vijana wa Jamhuri ya Ireland Kyle Fitzgerald kutoka Galway United, 18.

## GARNACHO APEWA TUMAINI

MILAN, Italia

**NAPOLI wamemuarifu winga wa Argentina mwenye umri wa miaka 20 Alejandro Garnacho kwamba watakuwa tayari kujaribu kumsajili tena ikiwa Manchester United itapunguza mahitaji yao.**

Steven Gerrard ameripotiwa kuomba kuondoka kwenye klabu ya Saudia Pro League Al Ettifaq baada ya miezi 18, kulingana na ripoti kutoka Saudi Arabia.

Torino ndio wanaopewa nafasi kubwa ya kumsajili kiungo wa kati wa Chelsea na Muitaliano Cesare Casadei, 22, huku Lazio sasa ikiwa nje ya mbio hizo.

Mjasiriamali spoti
MJASIRIAMALI JANUARI 31, 2025
Tovuti: www.mjasiriamali.co.tz



# SIMBA, YANGA ZATEGWA

NA MWANDISHI WETU

**FAHAMU kwamba mwenye kucheza na kutoa maelekezo ndani ya kikosi cha Yanga, Pacome Zouzoah ni pasua kichwa kutokana na uwezo wake kwenye kupiga pasi ndefu na fupi akiwa uwanjani.**


Nyota huyo kwenye dirisha dogo ilikuwa inatajwa kuwa yupo kwenye rada za mabosi wa Simba kwa kuwa mkataba wake unagota mwisho inaelezwa kuwa mabosi wa Yanga walifanya mazungumzo naye kuhusu kuboresha mkataba wake.

Hivi karibuni Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally aliweka wazi kuwa wanamfuatilia mchezaji huyo kwa kuwa wanatambua mkataba wake unakaribia kuisha wakiona anafaa watahangaika naye.

"Kuna mchezaji ambaye yupo pale ambaye ni Pacome huyu tunamfuatilia tukiona anatufaa basi tutahangaika naye kwa kuwa tunajua kwamba mkataba wake unaisha."

Pacome ndani ya ligi amecheza jumla ya mechi 14 kati ya 15 akikosekana kwenye mchezo mmoja akisepa na dakika 803 uwanjani akifunga mabao 5 na kutoa pasi tatu za mabao.

Yanga kwa sasa ipo kwenye maandalizi kuelekea mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Kagera Sugar mchezo unaotarajiwa kuchezwa Uwanja wa KMC, Complex, Februari Mosi 2025.




## WYdad bado ipo kwa Mzize

NA ASHA SEKEFU

**SIKIA! Timu ya Wydad Athletic ya nchini Morocco imeendelea kuwasilisha maombi ya kutaka kumnunua mshambuliaji wa Yanga, Clement Mzize, lakini sasa imeongeza ikisema pia inahitaji huduma ya Stephanie Aziz Ki.**



Katika taarifa iliyotolewa na Wydad inasema wako tayari kulipa ada ya Dola za Marekani 800,000 kwa kila mchezaji sawa na jumla ya Dola Mil 1.6 sawa na zaidi ya Bilioni 3.5 ili wajiunge na timu yao inayoshiriki Ligi Kuu ya Morocco.

Hata hivyo mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga imewajibu waarabu hao kuwa wachezaji hao hawauzwi kwa pesa yoyote ile.

Kocha Mkuu wa Wydad, Rulani Mokwena, ameieleza Bodi ya Wakurugenzi wa timu hiyo kuwa anawahitaji wachezaji hao ili kuongeza nguvu katika kikosi chake.

Mokwena alianza kuvutiwa na wachezaji hao tangu akiwa na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, ilipokutana na Yanga katika michuano ya CAF.